Toleo 14

# Ukweli wa Injili

*MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA KAZI YA KIMISHENI ULIMWENGUNI KOTE*

## UJASIRI WA YOHANA MBATIZAJI

*Hazina ya maelezo kutoka kwa (Marko 6:17-28.)*

Kicheko kikuu cha kejeli kilijaza ukumbi wakati Herode Antipa alikuwa akisherehekea pamoja na magavana, wakuu wa majeshi yake na viongozi wa ngazi za juu sana katika serikali yake. Sherehe hiyo ilikuwa ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwake. Mvinyo ulimiminwa, huku naye akiwa ananyanyuliwa na kushangiliwa kama kiongozi mkuu. Salome bintiye aliyemzaa na mke wa nduguye alicheza mbele ya wanaume akiwafurahisha kwa urembo wake.

Katika kuinuliwa kwake na kiburi cha wakati huo, Herode alimwita bintiye na kumwambia; "Uliza chochote unachotaka nami nitakupa, hata nusu ya ufalme wangu."

Akiwaza juu ya bahati yake, Salome alimwendea mama yake Herodia kwa ushauri. Herodia alikuwa amemwacha mume wake Herode Filipo ili kuishi na Herod antipa nduguye Filipo.Aliwazia hili kwa muda ili atoe ushauri kwa swali la bintiye. Antipa alikuwa amemzuru nduguye Filipo na akamtamani mkewe na kumpenda.Alimtongoza Herodia amwache mumewe ili waishi naye. Mke yule alikubali lakini kwa masharti kuwa Antipa pia naye amwache mkewe.



> "Si vyema kwako kumtwaa mke wa nduguyo."

Kwa kufuata mapenzi, raha na matarajio yatakayofuata, Wote wakatalakiana na wapenzi wao na kujiunga pamoja katika ndoa. Kwa hasira Herodia akakumbuka mtu aliyeitwa mtu wa Mungu, Yohana mbatizaji. Alikuwa amemkemea Herode Antipa na akatiwa gerezani. Umati ulikuwa umevutiwa na mahubiri yake kwa furaha. Huyo aliyeitwa nabii wa Mungu alimwambia Herode pamoja na watu kuwa "si vyema kwako kumtwaa mke wa nduguyo. Kwa uamuzi, Herodia akamwamuru Salome aitishe kichwa cha Yohana mbatizaji ili apewe. Herode alihuzunika lakini kwa kuwa alikuwa ameapa hadharani kutimiza ahadi yake; Papo hapo aliitisha muuwaji akamkata Yohana kichwa kule gerezani akamkabidhi Salome na Herodia.

Yohana mbatizaji mtangulizi wa Yesu Kristo alipoteza maisha yake kwa sababu ya ujasiri wa kusema kweli yote pasipokujali matokeo.Wakati viongozi wengine walipokuwa tahadhari wasije wakamkwaza kiongozi wao, Yohana alimtiii Mungu na kushiriki injili isiyochanganywa. Mwanaharakati wa kiyahuudi Josephus alishuhudia akisema; "Herodia aliamua kuvunja sheria za nchi yetu na kutalakiana na mumewe na

*(Endelia kwa ukurasa 2)*


| Mhariri 3 | Talaka na Ndoa 5-8 | Ukewenza Umeping Wa Je, na Watoto? 9 | Maswali na majibu 10-11 | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 12 |
|---|---|---|---|---|
| Wa Uchambuzi wa Biblia 4 | | | | |

# Mambo Ambayo

# BIBLIA

## Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35
**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21
**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10
**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6
**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11
**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8
**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22
**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36
**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18
**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4
**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, 1 Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17
**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16
**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, 1 Kor. 7:10-11
**Urembo wa Nje**
1 Tim. 2:9-10, 1 Kor. 11:14-15, Kum. 22:5
**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46
**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20
**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17
**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Endelea kutoka ukurasa 1)*

akaolewa na Herode Antipa ndugu ya mume wake kama angali hai hapo kando na babaye" (*Mambo ya mitazamo* 18:136.5).

Herode na Herodia walikuwa wakivunja sheria ya kiyahudi na ya Musa mara nyingi. Mtu wa Mungu alionekana kupuuza uovu huo mwingi, Lakini Mungu alikuwa amemtuma kuiandaa njia ya Bwana.

Jamii leo imejawa na maovu na giza la kiroho. Wanadamu siku hizi wanaishi katika enzi ya neema na na ukweli ambapo Yesu amesharejesha hadhi na usafi wa ndoa kati ya mume na mke mmoja maishani.Ndoa ya kiungu ni muundo wa Mungu lakini kanuni za kisiasa na za uhusiano zinasonga mbali sana kutoka kwa Mungu na mpango wake wa ndoa. Talaka na ndoa ya pili ni kinyume cha kanuni ya ndoa na kinyume na maagizo ya mungu katika agano la kale.

Wanaokiri kuwa wakristo, wengi wao wana ndoa za uzinzi ambazo zimeidhinishwa na makanisa mengi. Ukweli wa somo hili ni kero kwa wasiotubu likini utawafungua wafungwa, kuonya na kuelekeza kwenye usalama wale wanaothamini ndoa. Takia nini huja kwa wale wanaonyamaza kwa kuhofia kukwazwa.

Wako wapi akina Yohana mbatizaji wa siku hizi?

—mws


### UKWELI WA INJILI

Gazeti la 'Ukweli wa Injili' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa watu wote wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuhimiza wote katika ukweli wa neno la Mungu. Nakala hii hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu enzi za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ni sheria ya kipekee ya imani inayokubalika. Inafundisha wokovu na ukombozi kutoka kwa dhambi kupitia dhabihu ya Yesu Kristo msalabani na ujazo wa Roho Mtakatifu ili kuongoza, kuelekeza na kutia nguvu. Utakatifu unaonekana katika kila sehemu ya maisha, na umoja na utangamano wa watu wa Mungu; huduma inayokubalika kwa Mungu kupitia uhusiano wa kibinafsi wa upendo uliosimama kwa msingi wa ukweli.

Waandishi: Michael na Rene Smith

### UAGIJAJI

*Ukweli wa Injili* ni chapisho la kieletroniki la kila robo ya mwaka jinsi mungu anavyotuongoza. Tutazame katika mtandao wetu, www.thegospeltruth.us ili uagize kupitia orodha ya amwanipepe ili upokee toleo lako jisikie huru kutumia orodha ya majina na anwani pepe za wapenzi wako ambao wange penda kuagiza toleo hili kutoka kwa mwandishi.

### WASILIANA NASI

Gazeti la *Ukweli wa injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimisheni ambazo sisi hutenda huwezeshwa kupitia kwa matolea ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.



Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA

editor@thegospeltruth.org

# Tahariri



*"Maana mimi nakuchukia kuachana, asema Bwana Mungu wa Israeli; naye aifunikizaye nguo yake kwa udhalimu namchukia, asema Bwana wa majeshi; Basi jihadharini roho zenu msije mkatenda kwa hiana."* --Malaki 2:16

Mungu alikasirishwa baada ya kulea na kutunza wana wa Israeli, bado walimgeuzia mgongo na kufanya uzinzi wa kiroho kwa kuwafuata miungu wengine. Mungu aliwaumba wanadamu ili awe na uhusiano pamoja nao. Lakini katika dhambi, mwanadama alisababisha uharibifu na uchungu.

Mungu anachukia talaka. Kwa sababu yeye anaelewa majuto yaliyomo katika tendo hilo. Mzigo nilionao msimu huu ni juu ya somo la talaka na ndoa ya pili. Hadi ithibitishwe, 'talaka na ndoa ya pili' katika makala haya linaelezwa kuwa neno katika umoja sio wingi. Jinsi ilivyo katika masomo mengine, nina upungufu wa kufafanua kila hoja kutumia maandiko kuhusu somo hili. Ombi langu ni kwamba, Bwana atabariki makala haya na kutia ufahamu kila msomaji wa somo hili lililo muhimu katika karne hii ya dunia tunayoishi ndani leo.

Talaka na ndoa ya pili imekithiri mizizi sio tu kwa wasioamini bali kwa wanaokiri wokovu pia. Yesu anafundisha kwamba talaka na ndoa ya pili ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Watu wamejaribu kubatilisha maandiko ili kupata mwanya wa kuhalalisha ndoa ya pili kama mpenzi aliyeachwa angali hai. Niliwahi kusikia mhuduma mmoja wa ushirika wa kanisa la Mungu fulani akishuhudia baada ya kumwacha mkewe: "Mungu aliniambia hakuna haja niishi mpweke." Roho mtakatifu hatawahi kutuongoza kinyume na neno la Mungu.

Talaka na ndoa ya pili ni nguvu ya uharibifu katika ndoa ya jamii nyingi.Watoto ndio wanaojuta kwa sababu ya ubinafsi na dhambi ya wazazi. Mungu alikusudia watoto waishi na baba na mama pamoja. Watu wana tafuta mkato katika dunia hii yetu. Ikiwa kitu chema kitapatikana, ni sharti tuwe na nguvu na juhudi. Hakuna kinachoweza kufananishwa na ndoa itoshelezayo halisi ya mungu, Lakini lazima tuwe na kujitolea. Ndoa ya pili si suluhisho kwa ndoa iliyo matatani. Sasa ni wakati wa kuingia katika biashara na Mungu na tutafute neema kuu, upendo na msamaha.

Maisha yetu yote yameguzwa na talaka na ndoa ya pili kwa njia moja au nyingine. Ni wazi kuwa hatutaruhusu wingi wake kutuzuia kutangaza shauri lote la Mungu. Jinsi ilivyosemwa mwanzo ni kimya kitakacholeta kulegeza msimamo.

Ninahimiza kila mzazi, Mawalimu wa watoto kanisani, Mhuduma yeyote wa watoto na vijana; wafundishe haya mafundisho muhimu ya kweli. Ndoa ni ya maisha yote ya mtu na hawezi kuitupilia mbali kwa urahisi vile shetani anavyojaribu kuonyesha.Mungu ana mpango mzuri na ndoa. Ifanye katika njia ya Mungu!

Michael W. Smith

Oktoba 2015

mengi kwa

MTANDAO

*Tutembelee kwa*

*www.thegospeltruth.org*

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*



Funguo za ndoa ya furaha

*Penda*
*Sikiliza*
*Toa*
*Tukuza*
*Samehe*
*Kubali*
*Jitolee*
*Omba*
*Himiza*
*Amini*
*Heshimu*
*Saidia*

# MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

## Somo: TALAKA NA NDOA YA PILI

**Maandiko:** *Kila amwachaye mkewe na kumwoa mke mwingine azini; naye amwoaye yeye aliyeachwa na mumewe azini.* —Luka 16:18

**Hitimisho:**

Ndoa tangu mwanzo ilikuwa ni patano la maisha kati ya mume mmoja na mke mmoja. Patano hili lilinajisiwa na tama ya kuoa wake wengi, talaka na ndoa ya pili. Yesu alirejesha usafi wa ndoa. Ndoa nyingine kama mpenzi wako angali hai ni uzinzi.

---

### I. Hapo Mwanzo

A. Mwanzo 2:18 Mungu limuumbia Adamu msaidizi.

B. Mwanzo 2:23-25 Patano la mume mmoja na mke mmoja.

### II. Ndoa ya Jinsia Moja Haikubaliki

A. Walawi 20:13 Ni chukizo.

B. Warumi 1:26-32-Akili iliyopotoka.

C. Warumi 1:26-32-Akili iliyopotoka.

### III. Sheria ya Musa

A. Exodus 20:14 Mungu hakubali uzinzi.

B. Deuteronomy 22:22-29 Hukumu ya kifo kwa uzinzi.

C. Deuteronomy 24:1-4 Musa aliruhusu talaka.

D. Marko 10:2-5-Kwa ajili ya mioyo migumu.

### IV. Sheria ya Kristo

A. Marko 10:2-12

1. Ms. 6-7 Ndoa ni kati ya mume na mke talaka ilikataliwa tangu mwanzo.
2. Ms. 8-9 Ndoa isivunjwe.
3. Ms. 10-12-Talaka na ndoa ya pili ni uzinzi.

B. Luka 16:18 Yeye amwoaye aliyeachwa azini.

C. Mathayo 5:31-32 Kwa sababu ya uasherati.

### V. Sababu Maalum Za Ndoaya Pili

A. Warumi 7:1-3 Kifo huondoa agano la ndoa. Ndoa ya pili ni halali tu kwa wajane (Waume kwa wake).

B. I Wakorintho 7:10-11 Mkiachana, nyote sharti mbaki bila ndoa nyingine.

C. I Wakorintho 7:39 Kifo huweka huru; Oa/Olewa katika Bwana.

### VI. Hukumu Kwa Uzinzi

A. Waebrania 13-4 Mungu atahukumu.

B. Wagalatia 5:19-21 Kazi za mwili.

C. I Wakorintho 6:9 Hawataurithi ufalme wa Mungu.

D. Ufunuo 21:8 Watakuwa na sehemu yao katika ziwa la moto.

E. Yohana 8:3-11 Nenda na usitende dhambi tena.

### Hitimisho:

*Ndoa na iheshimiwe na watu wote na malazi yawe safi: kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.*

*—Wahebrania 13:4*

# TALAKA NDOA YA PILI

## Katika mwanzo wa nyakati,

**Mungu aliumba mwanadamu. Aliona si vyema huyo mtu awe peke yake nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye (Mwanzo 2:18). Basi Mungu akanzisha taasisi ya ndoa. Ilifanywa na kuwekwa wakfu na Mungu. "Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataaambatana na mkewe, nao watakuwwa mwili mmoja" (Mwanzo 2:24).**

Ndoa ndiyo uhusiano uliokaribu kuliko uhusiano mwingine kati ya wanadamu na wa pili kwa uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu mwenyewe. Ndoa ilianzishwa na Muumba; mpango wake ilikusudia ndoa kuwa ya maisha na patano la majukumu kati ya mume na mke. Kujamiana ni kipawa ambacho kimepeanwa tu kwa waliooana. Shetani amepigana na hadhi ya ndoa na amejitahidi kuangamiza jamii. Dunia imeondoa thamani na kulegeza msimamo pamoja na kuleta maana mpya ya ndoa. Hayo yote hayatabadili ukweli wa Mungu juu ya somo hili.

### Ndoa—Mume mmoja na mke mmoja

Ndoa ya kiungu ni kati ya mume na mke. Ndoa ya jinsia moja ni kinyume cha ndoa na ni chukizo kwa Mungu. Neno la Mungu linapinga ndoa ya jinsia moja (Walawi 20:13, Warumi 1:26-32) na inaeleza kuwa wale watendao mambo kama hayo hawataurithi ufalme wa Mungu (I Wakorintho 6:9).

### Sharia ya Musa


Katika sheria ya Musa, kama mke mgeni aliyeolewa angegunduliwa na mume wake ya kwamba hakuwa bikira, ilifaa apigwe na mawe hadi afe na kama alisingiziwa na mumewe, mume angemchukua kama mkewe na masharti kuwa "hana ruhusa ya kumwacha siku zake zote" (Kumbukumbu 22:19). Kama watu wawili wasioana wangepatikana katika uasherati, Yule mume ilibidi amwoe yule mke na pia hangemwacha siku zake zote (Kumbukumbu 22:29).

Sheria ya Musa ilisema wazi: "Usizini" (Kutoka 20:14). Kama mtu aliyeoa angepatikana akizini na mke mwingine, hukumu ilikuwa ni kifo kwa kupigwa mawe (au kunyongwa), Kwa kuwa Mungu hakutaka maovu katika Israeli (Kumbukumbu 22:22-29). Yule mkewe aliyesalia alikuwa sasa huru kuolewa kwa maana mumewe amekufa.

### Talaka iliruhusiwa chini ya Musa

"Baadaye kwa kuwaiga watu wa mataifa, Patano la ndoa lilianza kuwa legevu na mtazamo wa jumla kuhusu talaka ukaanza kuchukua mkondo mpya na hukumu ya kifo haikutolewa tena" (Maelezo katika *kamusi ya Smith*, *Uzinzi*) basi talaka na ndoa ya pili ikatapakaa kote. Musa alipeana ruhusa ya talaka katika agano la kale (Kumbukumbu 24:1-2) ambayo inasoma: "Mtu akiisha kutwaa mke kwa kumwoa, asipopata kibali machoni mwake, kwa kuwa ameona neno ovu kwake, na amwandikie hati ya kumwacha, akamtilie mkononi mwake na kumtoa katika nyumba yake. Naye akiisha kuondoka, katika nyumba yake, anaruhusa kwenda akawa mke wa mtu mwingine."

*(Endelia kwa ukurasa 6)*



—*Patrice Doolittle*

(Endelea kutoka ukurasa 5)

Wale ambao wamewahi kuoa au kuolewa mara ya pili kwa ajili ya sheria ya wanadamu, Sisi ni wenye dhambi machoni mwa Bwana wetu.
-Justin Martyr, 160 AD

### Kutoelewana juu ya sheria ya Wayahudi

Sheria ya Mungu inasema wazi kuwa aliyepatikana akizini afe kwa kupigwa na mawe lakini baadaye Musa akatengeneza njia ya talaka wakati kulikuwa na unajisi. Kulitokea ugomvi si haba kati ya wasomi wa kiyahudi wakati wa Yesu kuhusu sababu ambazo mke angepewa talaka kulingana na mtazamo wake. Mabishano yalitokana na tafsiri ya neno “unajisi” au ‘uchafu’ ambao ungeidhinisha talaka. Hakika kwa kusema, wayahudi walikuwa hafifu sana katika kutafsiri sheria ya talaka. Walimu wengi wangepeana talaka kama mume au mke amepatwa akizini, na wengine walilegeza msimamo na wangempa mume hati ya talaka ili amwache mkewe kama hakupata “kibali machoni mwake” Mume angepata hati kama mkewe ameunguza chakula jikoni au kuacha nyumba ikiwa chafu.

### Sheria ya Kristo

Mafarisayo walimwendea Yesu wakitarajia kumwingiza katika mjadala huo. “Je, Ni halali mtu kumwacha mkewe?” (Marko 10:2). Walikuwa wakiuliza kuhusu sheria ya Musa lakini kile Yesu alianza kuwafundisha kilirejesha taasisi ya ndoa katika sehemu yake katika uumbaji. Mafundisho ya Yesu yaliinua kiwango cha ndoa na haya ndiyo mafundisho yanayofaa tuishi kwayo enzi hii.

Yesu aliwauliza maana ya talaka kulingana na Musa , wakajibu: “Musa alitoa ruhusa kuandika hati ya talaka na kumwacha”(Marko 10:3-4). Yesu akawaambia “kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu aliwaandikia amri hii" (10:5). “Lakini tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, aliwafanya mume na mke...na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Basi alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe" (10:6-10). Tangu mwanzo wa wakati, talaka ilipingwa; ni lakini ilikuwa kwa sababu ya ugumu wa mioyo na dhambi ya mioyo ya wanadamu iliyofanya Musa kuruhusu. Hapa Yesu alifundisha kwamba, ndoa haifai kuvunjwa na mwanadamu. Hakuna sheria yoyote ya kidini au ya kiserikali inayofaa kuwa juu ya patano la ndoa mbele za Mungu. Aliwanyima haki waliyoitafuta katika sheria.

“Mume angepata hati kama mkewe ameunguza chakula jikoni au kuacha nyumba ikiwa chafu.”
[Tabia ya wayahundi]

### Ndoa ya uzinzi

Wanafunzi wa Yesu walionekana kung’ang’ana na jambo hili kama walivyo wengi leo. Walimuuliza Yesu tena juu ya jambo lili hili. Basi Yesu akanena sasa kwa ufasaha. “Kila mtu atakayemwacha mkewe na kuoa mwingine azini juu yake, na mke akimwacha mumewe na kuolewa na mtu mwingine, azini” (Marko 10:10-12). Andiko hili halingeeleweka bila kuchanganya maana. Yesu alisema wazi kuwa mtu akimwacha mkewe na kuoa mwingine azini, hii ni kwa sababu huyo mwingine hawezi kuwa mkewe wa ndoa na “ndoa” hiyo ni ya uzinzi.

Yesu aliendelea kufundisha katika (Luka 16:18): “Kila mtu atakayemwacha mkewe na kuoa mwingine azini juu yake, na mke akimwacha mumewe na kuolewa na mtu mwingine, azini.”

Si mume pekee ndiye anayezini bali pia mke. Ingawa mke hakutenda lolote, maana yeye aliachwa, anazini akiolewa. Yesu alifafanua kuwa yeye amwuoaye aliyeachwa azini. Bwana hataki ndoa ya pili ili tuwe na fursa ya kurudiana baada ya kuachana. Ndoa ni ya siku zote za maisha na katika macho ya Mungu itabaki vile bila kujali uhusiano na mapatano ya wanadamu. Yesu alirejesha agano la maisha la ndoa – agano aliloweka wakfu tangu mwanzo.

> "Ndoa ni ya siku zote za maisha na katika macho ya Mungu itabaki vile bila kujali uhusiano na mapatano ya wanadamu."

### Shikilia kuwa ni kwa ajili ya uasherati

"Imenenwa pia, mtu akimwacha mkewe, na ampe hati ya talaka: Lakini mimi nawaambia, Kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini" (Mathayo 5:31-32). Kulingana na historia ya kiyahudi, Hati ya talaka ilimruhusu aliyeachwa kuolewa tena. Hii ndiyo ilimfanya Yesu kusema, "Mume amfanya yeye kuwa mzinzi" Kama hakutenda jambo mbaya, mume wake angemshrikisha uzinzi akiolewa kwingine. Mume akimwacha mke kwa sababu ya dhambi ya ngono (hasa uasherati), hatawajibikia hilo mbele za Mungu kwa sababu alikuwa tayari mzinzi. Ingawa Yesu hakulaani kuachana kwa ajili ya uasherati, hakuacha nafasi ya ndoa ya pili.

### Ni kifo pekee kinachotenganisha ndoa

Mtume Paulo anafafanua juu ya ndoa ya pili. Ni kifo cha mpenzi pekee ndicho kinachomweka huru mwenzake kuoa au kuolewa. "Kwa maana mwanamke aliye na mume, amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai; hali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume. Basi wakati awapo hai mumewe; kama akiwa na mume mwingine huitwa mzinzi. Ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheia hiyo, hata yeye si mzinzi, ajapoolewa na mume mwingine" (Warumi 7:2-3). Hii inasisitiza hoja kuwa mtu akiolewa au kuoa tena akiwa na mpenzi (Mke/Mume) wake angali hai, anazini.

### Ukiachwa, baki bila kuolewa/kuoa

Kuna hali zingine za huzuni na bahati mbaya ambazo wake na waume hujipata ndani wakiwa pweke kwa ajili ya kuachwa na wapenzi wao ili waishi katika hali ya dhambi na uzinzi. "Mke asiachane na mumewe lakini ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, au apatane na mumewe; tena mume asimwache mkewe" (Warumi 7:10-11). Kama hali itazoroteka na kulazimu kuachana, wapenzi wabaki bila kuoa au kuolewa kama wangali hai wote. Mungu ana neema kubwa na atamfanya mtu kuishi peke yake na utakatifu kwa nguvu ya Yesu Kristo.

> "Uasherati ndiyo sababu pekee ambayo mtu anaweza kumwacha mkewe, lakini wakati angali hai,mume hana ruhusa kuoa mke mwingine. Wanawake hawaruhusiwi kuolewa na wanaume walioacha wake zao.Uhusiano kama huo si ndoa, lakini ni uzinzi."
>
> – St. Augustine

*(Endelia kwa ukurasa 8)*

(Endelea kutoka ukurasa 7)

> Ndoa ni uamuzi wa maisha... na kwa hivyo ni muhimu kwa wadogo na wakubwa kutambua ndoa kwa maombi na kutahadhari.

### Wapenzi wasiookoka

Paulo anazidi kutoa agizojuu ya kuishi na mpenzi asiyeamini. Anashauri kuwa kama mke anayeamini anaishi na mume asiyeamini, akiwa na haja kudumisha ndoa hiyo, asiache mumewe. Hakika kama mume anazini ni wazi kuwa hana haja ya kuishi na mkewe. Asiyeamini akiondoka, "Ndugu au dada huyo hayuko ndani ya kifungo kama hicho:

lakini Mungu ametuita katika amani (I Wakorintho 7:12-15). Anayeamini bado ana jukumu la ndoa hiyo mbele za Mungu lakini hayumo "kifungoni" au katika hatia ya lile tendo la asiyeamini (Tazama Mathayo 5:31-32). Kifungo hiki hakimweki yule mpenzi aliyebaki huru ili aoe au kuolewa. Paulo anatamatisha mlango huo akisema tena, "Mwanamke hufungwa maadamu mumewe yu hai, lakini ikiwa mumewe amefariki, yu huru kuolewa na mtu yeyote amtakaye; Katika Bwana tu." (I Wakorintho 7:39).

### Usioe wala kuolewa na asiyeamini

Ni muhimu kuzingatia kuwa hata kama ni ndoa ya kwanza au ndoa ya pili (halali), waliookoka hawafai kuoa na kuolewa na wasio okoka. "Oa au uolewa katika Bwana." Wengine wamepoteza wokovu wao kupitia ndoa nje ya imani. Mtoto wa Mungu, jihadhari, na usiache mapenzi yako yamwendee mtu asiyeokoka.

### Tumaini kwa mzinzi

"Ndoa na iheshimiwe na watu wote na malazi yawe safi; kwa maana washerati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu" (Wahebrania 13:4). Uzinzi ni kazi ya Mwili "watu watendao mambo ya jinsi hiyo, hawataurithi ufalme wa Mungu" (Wagalatia 5:19-21).

Yesu alikufa kwa ajili ya wazinzi, na kuna rehema na msamaha (Yohana 8:3-11). Mungu anampenda mzinzi bali anahitaji mtu huyo kuacha ushirika wa uzinzi. Ingawa kuna majuto ya dhambi, Roho Mtakatifu anaweza kuinua roho itubuyo katika sehemu ya utakatifu mbele za Mungu.

Maandiko ya agano jipya yanafundisha wazi ya kwamba ndoa ni patano lisilovunjwa. Talaka na ndoa ya pili si mpango wa Mungu kuhusu ndoa. Ndoa ni uamuzi wa maisha; na kwa hivyo ni muhimu kwa wadogo na wakubwa kutambua ndoa kwa maombi na kutahadhari kwa maana kuna fursa moja tu. Ndoa ni tukufu na ni Baraka kama mpango wa Mungu umefuatwa.

—mws

# Ukewenza Umepingwa

Ilikuwa tabia ya waume wengi katika agano la kale kuoa wake wengi (Ukewenza). Lakini mpango halisi wa kwanza wa Mungu ulikuwa mke mmoja na mume mmoja. Kristo alirejesha mpango wa awali wa Mungu katika agano jipya. “Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na amkewe; na hao wawili watakua mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja” (Mathayo 19:4-6).

“Wawili” haimaanishi watatu au wane. Hakika inamaanisha wawili. Mungu alimuumba mke mmoja, Hawa kwa Adam. Hakuumba ‘Maritha’ fulani ili kukamilisha ndoa. Ingawa ndoa ya wake wngi ingali katika mataifa mengi, hii ni kinyume na mpango wa Mungu.Kwa maneno machache tu, Yesu alikemea tendo hili na kurejesha uhusiano huu mzuri kupitia neema iliyokusudiwa tangu mwanzo wa dunia

Paulo kwa kumshauri Timotheo anaandika; “Basi imempasa askofu awe mtu asielaumika, mume wa mke mmoja...” (I Timotheo 3:2). Paulo hakuwa akilazimisha kuwa mtu lazima awe na mke, bali alikua akipinga ndoa ya wake wengi. Mtu hakuhitimu kuhudumu akiwa na wake zaidi ya mmoja. Kwa sababu alihitajika awe mfano mwema wa mpango wa Mungu kuhusu ndoa. ❖

# Je, na Watoto?



*“Lakini mtu yeyote asiyewatunza waliyo wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini” (I Timotheo 5:8).*

Mume au mke anapoachana na mwenzake na kuolewa na mwingine yeye anazini. Hii pia ni sawa kwa watu walioa wake wengi. Ni mpango wa shetani kuleta hali hizi na mtego wa kuzuia watu wasiokoke. Watu wakiokoka wanafaa kuacha dhambi zao na kuishi maisha ya utakatifu. Ndoa hizi za mchanganyiko zinaleta kuchanganyikiwa na kuumwa moyo. Kuna hali zingine ambazo zinaonekana ngumu kuzirejesha lakini kuna mwokozi anayeweza kupeana hekima na kugeuza hali hizo. Roho mtakatifu ataongoza katika ukweli wote na hatawahi kuongoza kinyume na neno la Mungu.

Mara nyingi watoto wamezaliwa katika ndoa za wake wengi na za uzinzi. Watoto hawa hawana hatia mbele za Mungu. Mtu akipeana moyo wake kwa Mungu na kujipima na kweli ya neno lake, atakuwa na tumaini la ndoa yake kuwa ndani ya mpango wa Mungu. Ingawa dhambi ni kukataliwa, haimaanishi mtu asilishe watoto wake, hata kama wamezaliwa katika ndoa isio ya kibiblia.

Paulo alisema kwamba, “Lakini mtu yeyote asiyewatunza waliyo wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini” (I Timotheo 5:8). Baba analo jukumu kuhakikisha ya kwamba watoto wake bila kujali kutoka kwa ndoa gani, hawajatunzwa tu kwa muda bali wametunzwa kwa vyote. Wanalipia gharama ya dhambi yake, na ni sharti mtu ajionyeshe katika kutii, kutunza na kulinda watoto hao.

Ni ushuhuda wa uchungu namna gani mtu kurudi kwake jioni na kumfurusha kwa mateke mkewe wa pili na wanawe, akijidai kuwa yeye ni mtu wa Mungu. Bado angali na jukumu kwa wanawe kama baba. Vilevile wanapoishi pamoja mkewe asiye wa halali lazima atunzwe katika hali ya kiungu. Ni vyema watu walio katika hali hiyo kutafuta ushauri kwa wanaume na wanawake wa Mungu. ❖

# MASWALI na MAJIBU

**Swali:** Je, unaweza kufafanua maandiko katika Mathayo 19:9 ambayo watu wengi hutumia kuunga mkono ndoa ya pili kwa ajili ya kukosa uaminifu?

**Jibu:** Itakuwa vigumu kuandika juu ya somo hili la talaka na ndoa ya pili kufafanua Mathayo 19:9 ambayo inasema: "Nami nawaambia, kila mtu atakayemwacha mkewe isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini: naye amwoaye aliyeachwa, azini."

Sheria ya msingi ya kutafsiri maandiko inajulikna kama "Muungano wa imani." Hii inamaanisha ya kwamba kuna uelewano na muungano wa maandiko na ya kwamba maanndiko hayapingani. Maandiko yaliyo magumu kuelewa yataeleweka katika kwa kulinganisha na yale yaliyo rahisi kuelewa. Kwa hivyo fundisho lisitoke tu kwa msitari mmoja pekee. Bali kwa muungano na ushirikiano wa maandiko mengine. Neno la Mungu halibishani lenyewe.

"Sheria ya msingi ya kutafsiri maandiko inajulikna kama 'Muungano wa Imani' Hii inamaanisha ya kwamba kuna uelewano na muungano wa maandiko na ya kwamba maandiko hayapingani."

Maandiko yako wazi kuwa ndoa ni ya maisha ingawa kunaweza kuwa na kuachana kutokana na kutoaminiana katika pingu za ndoa, ndoa ya pili kwa vyovyote kama mpenzi wa kwanza angali hai ni uzinzi mbele za Mungu. Maandiko katika Mathayo 5:32, Luka 16:18, Marko 10:11-12 na I Wakorintho 7:10-11, 39 yote haya ni wazi kwa somo hili. Kwa hivyo kutafsiri Mathayo 19:9 lazima maandiko hayo yatafsiriwe katika msingi huo.

Aya ya maandiiko yafuatayo yametolewa katika makala ya Ostis Wilson kuhusu somo hili:



> Kuelewa kwangu kwa maandiko haya ni kuwa yako na sehemu mbili. Mafarisayo walimuuliza Yesu kama ni halali mtu kumwacha mkewe kwa ajili ya jambo lolote (msitari 3). Huu ndio uliokuwa ukingo wa swali lao. Hawakuuliza lolote kuhusu kuoa mke mwingine baada ya kumwacha huyu. Hilo halikua swali miongoni mwao maana ilikuwa tabia yao ya kawaida, na talaka na ndoa ya pili ilikubaliwa na sheria. Hata walikuwa na zaidi ya mke mmoja na waliishi nao wakati mmoja (ukewenza).
>
> Katika sehemu ya swali hili, Yesu aliwajibu baada ya kunena kwa urefu mpango na kusudi la kwanza la Mungu kuhusu ndoa akishauri ya kuwa, sababu pekee ambayo mtu angemwacha mkewe ilikuwa ni uasherati. Hili linalingana na Mathayo 5:32 sehemu nyingine ambapo limetajwa jambo hilo likidhibitisha kuwa mtu anaweza kumwacha mkewe kwa sababu ya uasherati kwa sababu imeshudiwa na mashahidi wawili kwa maana katika neno la Mungu, kila neno linadhibitishwa kwa mashahidi wawili (Mathayo 18:16, Yohana 8:17). Kumwacha mke ndio jambo linalowatatiza hadi hapa tulipo. Sasa baada ya kujibu swali lao, aliendelea na kutambulisha fundisho lake ya kuwa mtu akimwoa mwingine baada ya kumwacha huyu, azini. Hili

> bila shaka liliwashangaza mafarisayo. Na pia si ajabu liliwashangaza wanafunzi wa Yesu hata kwa majibu yao: “Mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo, haifai kuoa” (Mathayo 19:10). Ni wazi kuwa wateule hawa walianza kuelewa ya kwamba ndoa ni patano la kudumu; na kama ni vigumu kutoka ndani namna hii, ni heri mtu asiingie.
>
> Kwa hivyo ninatamatisha kuwa, kulingana na Mathayo 19:9, mtu anaruhusiwa kumwacha mkewe kwa sababu ya uasherati pekee pasipo sababu nyingine. Na kuoa mke mwingine kama mke yule angali hai haikubaliki na kufanya hivyo ni uzinzi. Kwa maneno mengine yeye mume amekuwa akichangia hatia yake kwa kumwacha wakati alikuwa mtiifu na mwadilifu. Mungu atamhesabia hatia kwa kumfungua mkewe kwa hali hiyo ya uzinzi.

Neno ‘uasherati’ kwa kiyunani *pormeia* linamaanisha umalaya na ukahaba. Maana yake ni pana sana kuliko linavyotumika leo ambapo linaelezea tu kujamiana au ngono kati ya wawili wasioana. *Pormeia* linamaanisha dhambi yoyote ya ngono, bali uzinzi ni wakati yule aliyeoa au kuolewa hufanya mapenzi ya ngono na mtu asiye mpenzi wake halisi wa ndoa.

Kwa hivyo, ninatamatisha kuwa, kulingana Mathayo 5:32 na Mathayo 19:9, mtu anaruhusiwa kumwacha mkewe kwa sababu ya uasherati pekee pasipo sababu nyingine. Na kuoa mke mwingine kama mke yule angali hai haikubaliki na kufanya hivyo ni uzinzi. Kwa maneno mengine yeye mume amekuwa akichangia hatia yake kwa kumwacha wakati alikuwa mtiifu na mwadilifu. Mungu atamhesabia hatia kwa kumfungua mkewe kwa hali hiyo ya uzinzi. Kama ndoa ya pili ilikubalika, angetofautisha. Kila andiko la agano jipya linashikilia kuwa ndoa ni ya maisha yote bila kujali uasi wala dhambi ya wanandoa.

Mwandishi wa mambo ya mitazamo Mathew Henry aliandika yafuatayo kuhusu somo hili:

> Maumbile ya kifungo cha ndoa hakitegemei mapenzi na tabia ya wanandoa bali kinategemea tabia ya mwanzilishi wa kwanza na muundo huo. Kwa kuondoa utepetevu wa sheria ya Musa na kurejesha ndoa katika kiwango ilichokuwa mwanzo, Yesu hasisitizi tu hadhi ya agizo hili bali anazuia na kuziba mianya ya uovu kama mpango wa kutafuta visingizio vya uhuru kati ya mume na mke ili kutafuta ndoa nje na watu wengine.

*Maumbile ya kifungo cha ndoa hakitegemei mapenzi na tabia ya wanandoa bali kinategemea tabia ya mwanzilishi wa kwanza na muundo huo.*
*—Matthew Henry*

Tafsiri la agano jipya kwa jina *Emphatic Diaglot* linalotokana na makala *Vatican Linanukuu,* “Lakini nawaambia, kila mtu atakayemwacha mkewe isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yeye aliyeachwa, azini” (Mathayo 19:9).

Habari za somo hili katika Marko na katika Luka ni wazi bila mkanganyo wowote. Ni kwa bahati mbaya ya kuwa injili ya Mathayo iliandikwa hasa kwa wayahudi walioelewa tu matendo yao ya talaka na ndoa ya pili. Yesu aliwahutubia wayahudi kwa njia ambayo ilipeleka kumwelewa. Injili ya Marko ambayo iliandikiwa hasa Warumi na injili ya Luka ikaandikiwa watu wa mataifa ina ufasaha wa lugha kuhusiana na mafundisho ya Yesu juu ya somo la talaka na ndoa ya pili. Mathayo 19:9 inaelewana na sehemu zote za maandiko- Kumwacha mke na kuoa mwingine kwa sababu yoyote ni kinyume na mafundisho ya Yesu Kristo. ❖

JE, ULIJUA?

Katika agano la kale kulikuwa na muda mrefu wa kisheria wa kuchumbiana kabla wawili hawajaoana. Mapatano haya yalikuwa ya msimamo mkali kuliko yale ya nchi za magharibi. Kama kungepatikana na udanganyifu, mpango huo ungesambaratishwa kisheria kwa talaka. Katika sheria ya kiyahudi, kuchumbiana kulikuwa kama ndoa halali.

Ingawa wawili hawakuishi pamoja kama mume na mke, walihesabiwa 'kama mume na mke' jinsi ilivyokuwa kati ya Maria na Yusufu katika Mathayo 1:18-19.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# TUNZENI MOTO

**Anwani**

The Gospel Truth
605 Bishops Ct.
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

*Moto utatunzwa uwake juu ya madhabahu daima; usizimike.* —Walawi 6:13

Moto wa madhabahu uliounguza dhabihu haukustahili kuzimika. Moto haukuwaka pasipo kutunzwa bali ulitunzwa na kuchochewa. Kuni zilikuwa zisongezwe ili moto usizimike.



Ndoa nayo katika hali iyo hiyo, Mungu hataki moto wa mapenzi uzimike. Ili utakatifu wa ndoa udumishwe, lazima itunzwe. Ndoa nyingi zimeshika ubaridi kwa sababu wapenzi hawajachukua muda wao kuchochea uhusiano kwa upendo na kujitolea.

Ni rahisi watu kutekwa na kazi pamoja na shughuli za maisha, na kama wahuduma ni rahisi kutekwa na kazi ya Mungu. Ni muhimu kwa wahuduma kutunza moto wa ndoa. Adui ameweka mitego na wahuduma wengi wamepoteza njia zao kwa kukosa kutunza moto wa ndoa.

Ndoa ya mhuduma iliyotunzwa husaidia mhuduma kunawiri katika huduma yake ya injili. Mhuduma hana budi kutunza moto wa ndoa yake. Itakuwa baraka si tu kwa mhuduma na nyumba yake bali pia kwa kazi ya Mungu.

Tafuteni muda wa kushinda pamoja jioni moja. Fanyeni matembezi na mwende pamoja kwenye chakula cha jioni, chezeni mchezo, wachaneni na mazungumzo ya biashara, na ya kanisa na mwelekeze mawazo yenu tu katika kuwa pamoja.

**TUNZENI MOTO!** ❖

—mws

# Kutoka Moyoni Mwangu...



NYONGEZA YA UKWELI WA INJILI TOLEO LA 14

**KUPEANA TALAKA NA MTU KUOA TENA**

"Kama watoka kwa nyumba iliyovunjika jua kwamba wewe ni mtu muhimu sana anayestahili upendo."

## Watu kutokuwa waaminifu na kutalakiana ni jambo

ambalo linaleta majonzi mengi ulimwenguni. Hakuna maneno ambayo yanatosha kueleza uchungu wa ndani ambao mume au mke, pamoja na watoto, huwa nayo maishani wakati baba, mama, mume, au mke wameachana. Wake na waume hao, pamoja na watoto wao, huwa na masumbufu mengi maishani mwao kwa kusumbuliwa na hisia za kusalitiwa na wazazi wao, huku wakikazana na maswala ya kujihisi kwamba hawafai, hisia za kukataliwa na watu wale wengine, kupoteza tumaini maishani, na hasa hisia kwamba hawapendwi. Wakati mwingi wahusika hawa wa ndoa iliyovunjika hubeba hisia za kuhukumiwa na aibu ambazo kwa kweli zinastahili kuwa na yule mhusika ambaye aliwaacha.

Wewe fikiria kuhusu uchungu na masumbufu ya moyo ambayo mke au mme huhisi anapofikia mahali pa kufanya uamuzi kwamba hana budi kumwacha mume au mke ambayo amekosa kuwa mwaminifu ama ambaye anamdhulumu. Vitanda vya wengi hao huwa vimejaa machozi yanayomwagika usiku kucha kutoka kwa waume, wake au watoto wenye upweke ambao wana shauku kubwa ya kuwa na utimamu unaoletwa na familia inayopendana. Siku za usoni zinaonekana kujaa giza na ukosefu wa tumaini kwa wengi wa wake hao, waume, au watato ambao wameachwa upweke. Ulimwengu umejaa baba walioachwa peke yao na wake ambao wanajikaza kisabuni kuendelea kudumisha maisha ya familia kwa ajili ya watoto wao—huku wakiendelea kulemewa na mizigo ya kifedha.

Kama wewe watoka kwa nyumba iliyovunjika jua kwamba wewe ni mtu muhimu anayestahili upendo. Unaye rafiki ndani ya Yesu ambaye atatembea nawe kupitia kwa dhoruba na hali tofauti za maisha na misukosuko yake.

Kutalakiana na wahusika kuoa tena silo jambo ambalo linavunja ndoa tu mbali pia linatoa nafasi kwa kuvunjika kwa mahusiano ya jamii nzima, makusanyiko ya kanisa,

na pia mahusiano mengine ya wahusika. Wakati ambapo watu wameanza kulaumiana mmoja kwa mwingine kwa sababu ndoa imevunjika ndio wakati ambao Mkristo anastahili kusimama wima katika ukweli—kuwapenda wahusika wote wa ndoa hiyo bila kujaribu kutoa vizingizio kwa dhambi ambayo imetendwa na marafiki au familia.

Kuna mahusiano na ndoa nyingi za mchanganyiko. Mtu anapookoka na kuanza kuelewa mapenzi yake Mungu kwa ndoa, jambo hilo linaweza kuleta masumbufu moyoni na hali ya kuchanganyikiwa hasa ikiwa kulikuwa na watoto katika ndoa hiyo "ya pili." Basi mipango na mapenzi ya Mungu ni yapi katika hali kama hiyo? Kwa kweli hakuna mhudumu wa Injili ambaye anaweza kumpatia mtu neema ya kuacha mahusiano ya uzinzi ambayo mtu amekuwa ndani yake kwa miaka mingi na ambayo pengine mtu aliingia wakati alipokuwa mpumbavu wa kujua mapenzi ya Mungu kwa sababu alikuwa bado hajaokoka. Ni nguvu za Mungu tu ndizo ambazo zinaweza kumwezesha mtu kufanya maamuzi bora katika hali kama hiyo.

Mimi ninakumbuka nikiwa nimekaa kando kando ya  mke na mume ambao walikuwa katika hali kama hiyo. Mke wa mwanaume huyo alikuwa amemwacha na kuanza kuishi maisha ya dhambi. Basi mwanaume huyo akaoa tena na akapata watoto wengine na "mke wake wa pili." Halafu ndipo watu hao wawili wakaokoka. Huku wakiwa na majonzi mengi waliniuliza swali lifuatalo: "Sasa tufanyeje?" Ndipo nikawaambia mpango wa Mungu kuhusu ndoa, nikawahimiza wamkaribie Mungu na kuwahakikishia kwamba Roho wa Bwana atawaongoza katika swala hilo. Pia nikawaambia kwamba walikuwa wamekaribishwa kuhudhuria ibada za kanisa letu na kwamba sisi tulitaka wawe wakifika humo kanisani, hata ingawa pia niliwaambia kwamba hawangeza kushika wadhifa wa uongozi kanisani. Lakini kulikuwa na mwanaume mwingine ambaye alinipatia msukumo mkubwa ili niseme eti ndoa yake ilikuwa halali kwa sababu aliingia ndani mwake wakati akiwa kwenye "hali maalum." Nami nikamwambia kwamba kile alichohitaji sio mimi kuhalalisha ndoa yake mbali alihitaji kuwa na uhakika kwamba yeye alikuwa na huru mbele zake Mungu. Mimi kamwe sitamhukumu mtu yeyote, lakini sisi sote tutahukumiwa na Mungu kulingana na Neno lake.

Basi mimi nimekutana na watu wengi wazuri ambao maisha yao yameingia mashakani kwa sababu ya kuingia kwenye mahusiano ambayo hayalingani na maandiko, wakiwa wangali vijana. Moyo wangu umejaa majonzi kwa sababu ya watu kama hao. Kwa kweli mimi sina majibu yote, lakini najua kwamba kuna Mungu wa upendo, nalijua Neno lake,  na najua kwamba Mungu huyo atakuwa mwaminifu kwa kila mtu.

Ni jambo muhimu kwamba watu walioko katika hali kama hizo za kuvunja moyo na ambao wanataka kufanya mapenzi yake Mungu wasichukizwe na huduma ya Injili wakati ambapo injili hiyo inafunza kuhusu usafi wa Neno la Mungu kuhusiana na swala la ndoa. Kanisa la Mungu litaendelea kuuhubiri ukweli. Na kama wewe uko kwenye ndoa ya uzinzi hebu jua kwamba sisi tutaendelea kukupenda na kuomba pamoja nawe ili upate neema na nguvu za Mungu ili utembee katika mwanga wake.



Michael W. Smith

"Najua kwamba kuna Mungu wa upendo, nalijua Neno lake,  na



najua kwamba Mungu huyo atakuwa mwaminifu kwa kila mtu."